# UTHENGA WABWINO WA CHOONADI

Malangizo ndi Chilimbikitso kuchokera m'Baibulo kupita kwa amene akulalikira Uthenga Wabwino

## JIRANI YANGU NI NANI?

Mwanasheria mmoja alimjia Yesu na kumjaribu kwa kumuuliza: "Je, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele" (Luka 10:25-37). Yesu akamwambia, "Imeandikwa nini katika torati?" Mwanasheria akamjibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Yesu naye akamjibu, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi."

Mwanasheria huyo alikuwa Myahudi, na wakati huo viongozi wa kiroho wa Wayahudi waliamini kwamba majirani wao walikuwa ni Wayahudi tu. Ndipo wakachukulia kwamba wajibu wa kumjali jirani haukuwa uwafikie watu wa Mataifa, na hasa Wasamaria, ambao Wayahudi waliwachukua kuwa "mbwa" na "chotara." Wayahudi waliwachukia Wasamaria sana, hivi kwamba wao wangeweza kuvuka Mto Yordani, na kufuata njia ndefu zaidi, ili wasipitie nchi ya Wasamaria; ili kuepuka kabila hilo ambalo walilidhihaki sana.

Ni katika mandhari hiyo ndipo Yesu alisimulia kisa hiki kinachojulikana (kama) "Msamaria Mwema."


Mwanaume mmoja wa Kiyahudi alikuwa akisafiri kutoka Yerusalemu hadi Yeriko, wakati alivamiwa na wezi, ambao walimchapa na kumnyang'anya mali yake, wakamvua nguo, na kumwacha nusu-mfu kando ya barabara. Ndipo kuhani mmoja, mtu aliyetengwa kwa ajili ya kazi ya Mungu akamwona mtu huyo aliyeumizwa, lakini akamuepuka kwa kupitia upande mwingine wa barabara. Baadaye Mlawi naye akaja kupitia barabara hiyo. Akamtazama mtu huyo mwenye majeraha yaliyojaa damu, akamchungulia, lakini pia akapita upande mwingine wa barabara. Lakini Msamaria mmoja, mtu ambaye alichukiwa na Wayahudi, alipita barabarani humo.

Alipomtazama Myahudi aliyekuwa uchi na aliyejaa majeraha akamwonea huruma sana.

Basi Msamaria huyo akamwosha mwadhiriwa, akamtibu na kuweka bandeji kwenye majeraha ya Myahudi huyo. Halafu akampandisha kwenye punda wake na kumpeleka mpaka kwenye nyumba ya wageni. Hapo akamlipa mwenye nyumba malipo ya malazi ya Myahudi huyo, na hata gharama ya kumlisha, na akaacha maagizo kwamba amtunze. Akamhakikishia mwenye nyumba kwamba kama gharama nyingine ingetokea katika kazi hiyo ya kumtunza Myahudi, yeye angelipa wakati atakaporudi.

Alipomaliza kuhadithia kisa chake Yesu akauliza, "Katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?" Mwanasheria akamjibu, "Ni huyo aliyemwonea huruma." Basi Yesu akamaliza kisa chake kwa kumhimiza na kumpa changamoto mwanasheria huyo kwamba: "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo."

Kama watoto wa Mungu sisi sote tumeitwa ili tuwe na moyo na mawazo ya Msamaria mwema. Katika utamaduni uliojaa ubaguzi na kiburi cha Wayahudi dhidi ya Wasamaria, Msamaria ndiye alihudumu upendo na pia mahitaji ya Myahudi. Ni jambo la kushangaza kwamba, Yesu hakunena kuhusu Myahudi akimsaidia Msamaria. Basi kwetu sisi watoto wa Mungu, haijalishi kama tumezaliwa kwenye kikundi kinachodharauriwa, au kutoka kile kinachodharau watu wale wengine. Sote tunahitaji kuwa na huruma na upendo kwa kila mtu, bila kujali kabila lake, cheo cha kijamii, taifa lake, dini, rangi ya uso wake, au familia yake. Hii ni moja ya mwongozo wa maisha ya Ukristo, na ni jambo ambalo linahitaji kuwatofautisha watu wa Mungu kutokana na jamii na tamaduni ambazo wamezaliwa ndani mwake. ■



"Sote tunahitaji kuwa na huruma na upendo kwa kila mtu, bila kujali kabila lake, cheo chake cha kijamii, taifa lake, dini, rangi ya uso wake, au familia yake."


Urembo Unaotokana Na Maumbiile Tofauti Tofauti 2
Tahariri 3
Mwongozo wa Kujifunza Biblia 4
Usawa wa Wakristo Ukilinganishwa na Uonevvu 5-6
Maswali na Majibu 7
Je, Wajua? 
Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

# UREMBO UNAOTOKANA NA MAUMBILE TOFAUTI TOFAUTI

Mungu alipovitazama vitu vyote alivyoumba aliona kwamba kila kitu, "ni chema sana" (Mwanzo 1:31). Miti, miti-shamba, maua, viumbe vya barahani, na hata wanyama, walikuwa tofauti tofauti, na wenye rangi-rangile. Maumbile yenyewe yanatuonyesha kwamba Mungu anapenda utofauti wetu. Wanadamu nao wako vivyo hivyo. Mungu aliumba kila mmoja wetu kwa njia ya kipekee, kwa maana hamna watu wawili duniani ambao wanafanana kabisa kabisa.

Wanadamu wana tofauti ya maumbile, tofauti ya mambo wanayopenda, nguvu tofauti, na hata urembo tofauti. Ukiongeza utofauti wa watu binafsi, kuna kabila na tamaduni tofauti tofauti kati ya watu ambao wametapakaa kote ulimwenguni. Basi utofauti wetu si jambo ambalo watoto wa Mungu wanahitaji kuhofu, bali tunahitaji kulikaribisha na kulifurahia. Hata ingawa watu wote wako sawa machoni pake Mungu, maumbile ni ya kupendeza zaidi kutokana na utofauti wetu wa maumbile. Wakristo wanahitaji kufurahia urembo wa maumbile ya Mungu wa kuumba wanadamu walio tofauti tofauti.

Hakuna shida kwa makabila tofauti tofauti kuheshimu na kutunza urithi wao wa kitamaduni, mradi tu kwamba hawadunishi urithi na utamaduni wa watu wale wengine. Lakini ni makosa kwa ulimwengu wetu wa sasa kuendelea kutilia mkazo umuhimu wa tamaduni tofauti tofauti, kwa misingi ya mitazamo ya kilimwengu, ambayo inatokana na ubinadamu, badala ya msingi unaotoka kwa Mungu. Wakristo wanaweza kupenda na kufurahia urithi wa makabila yao tofauti tofauti, na hata tamaduni zao, bila ya wao kuingia kwenye mtego wa kusema kwamba maadili yote yako sawa; jambo ambalo ndilo linatiliwa mkazo sana na dhana za kilimwengu zinazosema kwamba tuzishereherekee tamaduni zetu tofauti tofauti.

Basi tamaduni za jamii tofauti zinahitaji kufurahiwa, huku kukizingatiwa kwamba imani zote pamoja na mambo yanayotiliwa umuhimu kwenye jamii hayako katika mstari wa mbele wa maadili ambayo yanastahili kuongoza maisha yetu. Injili haikuhubiriwa ili iangamize utamaduni, lakati wakati mienendo yetu ya kitamaduni yanaenda kinyume na Neno la Mungu, Wakristo wanahitaji kuishi kwa miongozo tofauti; wanahitaji kuupatia ukweli wa Mungu umuhimu zaidi. Kuna urembo unaopatikana kutokana na maumbile tofauti tofauti ya wanadamu, wakati ambapo maumbile hayo yanaambatana na utakatifu wake Mungu. ■

"Twamwomba Mungu aharakishe siku ambayo ubaguzi wote utaondolewa, siku ambayo kila nafsi ambayo Kristo alikufa kwa ajili yake itaweza kutambuliwa kuwa yenye thamani machoni pake."

--F. G. Smith (Mchungaji mwanzilishi wa Kanisa la Mungu, 1901)

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri




*Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo.* —Mathayo 7:12

Ulimwengu wetu unaweza kuwa mahali bora zaidi kama watu wangeweza kufuata kanuni hii rahisi ya maisha: Kwamba tumfanyie kila mtu kile ambacho tungependa kufanyiwa. Lakini habari za kilimwengu zimejaa ubaguzi, chuki, ukosefu wa msamaha, kutengwa kwa watu, ubaguzi wa rangi, na hata migogoro. Lakini mimi nina furaha kwamba, Yesu Kristo hakutufundisha tu kuhusiana na njia bora ambayo mwanadamu anaweza kufuata, bali pia Yeye hutupatia neema na upendo wa kiungu wa kuwapatia watu wa tabaka na makabila mbali mbali, na hivyo akatuwezesha kuishi kwa amani na utangamano.

Somo la toleo hili la Ukweli wa Injili ni "Usawa wa Kikristo." Mungu alituumba sisi sote tukiwa sawa, na kwa hivyo hata ingawa lugha, mianzo yetu, rangi zetu, n.k., ni tofauti, sisi kama Wakristo tunahitaji kuwapenda watu wote na kumpa kila mtu heshima zake.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Nilipokuwa natafakari kuhusu somo hili nilikuwa na wazo kwamba nitafute waandishi kutoka nchi na mataifa mbali mbali, ili waweze kushiriki kwenye maandishi haya. Kwa kweli katika nchi nyingi ulimwenguni kuna maswala ya maonevu yanayotokana na ubaguzi wa rangi, ukabila au hadhi ya watu katika jamiii hizo n.k. Ni kweli kwamba sisi hujifunza mtu mmoja kutoka kwa mwingine, na kuna faida inayoweza patikana kutokana na watu tofauti kusema kuhusu mambo yaliyo kwenye mandhari waliyo ndani yake. Lakini Bwana akanileta kwenye ukweli huu: kwamba sisi sote tuna mawazo, hisia, na hata hadithi tofauti ambazo tunaweza kusimulia, lakini ukweli (kamili) hautegemei hadithi yangu, au hata hadithi yako. Neno la Mungu ndilo kipimo kifaacho cha ukweli, na ndilo ambalo linahitaji kupima mambo yote, bila kujali mawazo na fikira zetu za kibinafsi. Ni jambo la kuhuzunisha sana wakati Mkristo anapokuwa mwaminifu zaidi kwa kabila na tamaduni zake, badala yake kuwa mwaminifu kwa imani ya ya Kristo.



Watu wengi hutoa vijisababu tofauti tofauti kwa ajili ya mielekeo na tabia zao, huku wakitumia ujuzi wao wa kibinafsi katika swala hili. Lakini hebu Bwana atusaidie kutazama kioo cha Neno la Mungu ili tukitumie kuyachunguza maisha yetu. Kusema kweli watu wote hawatendewi kwa njia ya haki na kwa heshima wanazostahili, jambo linatokana na dhambi zake mwanadamu. Kuna maonevu, ubaguzi wa rangi, na kutowatendea watu wale wengine haki kwa misingi ya utajiri, rangi za nyuzo zao, kabila zao, na vyeo vyao vya kijamii. Jambo hili liko huku Marekani ya Kaskazini na hata ya Kusini, Bara Uropa, Bara Asia, na hata katika Bara Afrika. Lakini haijalishi ni ubaguzi wa aina gani tunaokutana nao, Wakristo wana jukumu la kuwapenda na kuwapa heshima watu wote. Hatustahili kuingiza ubaguzi na kinyongo kilichoko katika jamii kwenye Kanisa la Mungu; badala yake tunahitaji kuishi kwa viwango vilivyo vya juu zaidi ya mambo ya kijamii, kwa neema yake Mungu. Mkristo anapokumbana na matendo yasiyo ya haki, na hata kupatwa na maumivu moyoni kwa ajili ya jambo hili, yeye anahitaji kuleta jambo hili kwa Bwana.

Ni makosa kumhukumu mtu au kumfanyia mambo yasiyo sawa kutokana na rangi yake ya uso, awe ni mweusi, wa kahawia, au mwekundu. Lakini kikawaida, ni rahisi sisi kukubali kwamba tajiri hastahili kumwonea mtu maskini, na kwamba mamlaka ya kabila lenye nguvu yasitumiwe dhidi ya kabila ambalo ni nyonge. Lakini pia ni muhimu kwamba maskini asimwonee tajiri, na kwamba kabila ndogo lisionee kabila lenye nguvu zaidi za kisiasa.

Hata ingawa ujuzi wangu unaweza kuwa tofauti na wako, kwa kweli mimi nishawahi kosa kufanyiwa mambo yasiyo ya haki, nikaonewa, na kupata kuhadaliwa kutokana na rangi yangu ya mwili, hapa hapa nyumbani, na hata katika nchi za ng'ambo. Mambo haya nimeyapatia kutoka kwa watu wanaojiita Wakristo, na pia kutoka kwa wenye dhambi wa ulimwenguni huu. Lakini wakati machungu yalizuka moyoni mwangu kwa sababu ya kutotendewa haki, Mungu alinijulisha kwamba nilihitaji kusamehe badala ya kuwa na kinyongo. Haya ndiyo mafundisho ambayo yanapatikana katika Biblia!

Sisi kama Wakristo hatustahili kujipima kwa vipimo ambavyo ulimwengu umeweka, lakini tunahitaji kuwatendea wote ambao wametukosea kwa njia ya upendo na msamaha. Basi hebu Mungu atusaidie sisi watu wake ili tuishi pamoja kwa umoja.

Michael W. Smith

Oktoba, 2023



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Usawa wa Wakristo (Uonevu)

**Masomo ya Maandiko:** *Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu.* —Wagalatia 3:26-28

**Maana:** Maana ya uonevu ni kuwatofautisha watu wawili au zaidi, au kutofautisha vitu (Vocabulary.com). Lakini kwa kweli neno uonevu hutumiwa kuonyesha hali ya watu wa kikundi kimoja kukosa kutendewa mambo kwa njia ya haki, au kutendewa kwa njia ya ubaguzi.

**Muhstasari:** Watu wote wameumbwa na Mungu, na wako sawa mbele zake Mungu. Injili ilitolewa kwa ajili ya watu wa lugha zote, bila kujali rangi, kabila, utaifa, na hali zao za kiuchumi au vyeo vyao vya kijamii. Wakristo wanastahili kuwa na umoja, na wanatakiwa kuwapenda watu wote, na kwamba wasiishi kwa misingi ya uonevu, ukosefu wa msamaha, au kwa jinsi ambavyo walimwengu huwabagua wenzao.

### I. Tumeumbwa na Mungu

A. Mwanzo 1:127 Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake Mungu.
B. Malaki 2:10 Sote tuna baba mmoja.
C. Matendo 17:26 Watu wa mataifa yote chanzo chao ni kimoja.
D. Mitume 22:2 Bwana aliwaumba matajiri pamoja na maskini.

### II. Injili ya Watu Wote

A. Yohana 3:16 Mungu apenda watu wote.
B. Wagalatia 3:26-28 Wote tu wana wa Mungu.
C. Ufunuo 14:6 Injili yahubiriwa kwa mataifa yote ya watu.
D. Ufunuo 5:9-10 Watu wakombolewa kutoka kwa mataifa yote.
E. Warumi 10:12 Hakuna tofauti kati ya Wayahudi na Wayunani.

### III. Mungu Hawapendelei Watu

A. Matendo 10:34-35 Mungu hampendelei mtu yeyote. (Tazama pia Warumi 2:11).
B. Yakobo 2:1-10 Kuwapendelea na kuwabagua watu ni dhambi.

### IV. Ukuta wa Kugawanya Watu

A. Waefeso 2:11-19 Kigawanyishi kati ya Wayahudi na Watu wa Mataifa kimevunjwa. Sisi sote ni raia kwa pamoja.
B. Matendo 10:28 Mtu yeyote asiitwe najisi.
C. 1 Wakorintho 12:25 Kusiwe na mgawanyiko katika mwili.

### V. Tu Wamoja Katika Kristo

A. 2 Petro 3:18 Kua katika neema.
B. Waebrania 4:16 Msaada kutoka kwa kiti cha neema.
C. 2 Wakorintho 12:9 Neema ya Mungu yatosha.

### VI. Umoja

A. Yohana 17:10-22 Yesu anaombea umoja.
B. Zaburi 133:1-3 Dumuni pamoja kwa umoja.
C. Wafilipi 2:3-5 Tuhesabu wenzetu kuwa bora kutuliko.

### VII. Upendo Kati ya Ndugu

A. Yohana 13:34-35 Amri ya kupendana.
B. 1 Wathesalonike 3:12-13 Kuongeza na kuzidi katika upendo.
C. 1 Petro 1:22 Mpendane kwa moyo safi.
D. 1 Petro 3:8-9 Mhurumiane; mpendane kama ndugu.
E. 1 Yohana 3:14-18 Asiyependa ndugu yake hudumu mautini.

### VIII. Kuwafanyia Watu Hukumu za Haki

A. Walawi 19:15 Maskini na wenye nguvu uwahukumu kwa haki.
B. Yohana 7:24 Msihukumu kwa mtazamo wa macho tu.

### IX. Msimamo wa Mtu Binafsi Dhidi ya Ubaguzi

A. Marko 11:25-26 Wasamehe watu dhambi zao.
B. 1 Wathesalonike 5:15 Msilipe mabaya kwa mabaya.
C. Luka 6:27-28 Pendeni, ombeni, fanyeni mema.
D. Waebrania 12:14-15 Jichungeni dhidi ya mizizi ya kinyongo.

### X. Sisi Sio wa Ulimwengu

A. Johna 17:15-17 Tuko ulimwenguni lakini sisi sio wa ulimwengu.
B. Warumi 12:2 Msiifuatishe namna ya dunia.

Tamati

*Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.* —Wafilipi 2:3-5



# USAWA WA WAKRISTO UKILINGANISHWA NA UONEVU

Mafundisho ya Yesu Kristo yana umuhimu kuliko tamaduni zetu na taratibu za kizazi hiki. Katika ulimwengu ambao tangu zamani chuki, migogoro, ubaguzi na uonevu zimekita mizizi, kuna wito mwingine wenye nguvu ambao unatuweka huru na kutupatia ujuzi wa kutenda mambo kwa upendo, kuwahurumia watu wale wengine, kuwasamehe, na kuwatendea kwa njia ya usawa.



## Tumeumbwa na Mungu

Hata ingawa kuna kabila, utaifa, lugha, rangi, na hadhi tofauti za kijamii, sisi sote tumeumbwa na Mungu na sote tu sawa machoni pake. Sisi sote tuliumbwa "kwa mfano wake . . . mwanamume na mwanamke aliwaumba" (Mwanzo 1:27). Lakini kutokana na dhambi kumekuwa na watu tofauti kote ulimwenguni katika kila kizazi, ambao waliwatendea vibaya wale wengine, kibinafsi na kwenye makundi ya watu, kwa sababu ya wao kuwa tofauti. Lakini kwa kweli sisi sote tuna baba mmoja, na ni Mungu "alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote" (Matendo 17:26). Na hata ingawa familia ya kibinadamu huwa ni tofauti, sio tu kwa wanavyoonekana kimwili, bali hata kwa maumbile yao ya ndani, kwenye tamaduni zao, sheria zao, na mambo wanayotilia umuhimu; chanzo kamili cha watu wote duniani ni kimoja. Kama vile Methali 22:2 inavyosema: "Tajiri na maskini hukutana pamoja; BWANA ndiye aliyewaumba wote wawili." Sisi sote ni ndugu na dada, na hivyo tunastahili kuheshimiana na kuishi pamoja kwa umoja na masikizano.

"Kamwe wakristo hawastahili kuwapendelea watu au kuwabagua, bali wanahitaji kuwapenda na kuwaheshimu watu wote."

## Injili ya Watu Wote

Injili ya wokovu na tumaini ilitolewa kwa watu wote. "Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu" (Yohana 3:16). Upendo mkuu wa Mungu unawajumuisha watu wa tabaka zote, na Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote. Mtume Yohana alinena kuhusu malaika ambaye alitangaza injili ya milele kwa "hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa" (Ufunuo 14:6). Naye mtume Paulo aliandika na kusema, "Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu . . . Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:26-28).

## Mungu Hampendelei Mtu Yeyote

Mtume Petro, ambaye kweli alielewa vizuri mgawanyiko uliokuwako kati ya Wayahudi na watu wa Mataifa, alinena ukweli wa kudumu. "Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye" (Matendo 10:34-35). Mtume Paulo naye anasema kuhusu ukweli huo katika Warumi 2:11, "Kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu." Mungu anawapenda watu wote na hampendelei mtu yeyote. Yeye ana msimamo dhabiti wa usawa, na kamwe hampendelei mtu yeyote kutokana na utajili wake, kwa jinsi anavyojulikana, kwa ajili ya rangi ya uso wake, lugha yake, au hata familia yake. Wakristo hawana budi kuwa na roho na mwelekeo huo kwa watu ambao wako tofauti na wao. Mtume Yakobo naye alishughulikia swala hilo katika sura ya pili ya kitabu chake. Kama tajiri na maskini wameingia kanisani, na tajiri anapewa heshima kuu zaidi, si huo ni uonevu? "Mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi" (Yakobo 2:1-10). Mafundisho haya ni ya moja kwa moja, na yametolewa kwa ajili ya Wakristo wote katika siku zetu. Ukweli wa Neno la Mungu unahitaji kufanyishwa kazi mahali kote ambapo kuna tabia hizi za kuwaweka watu kando, kuwabagua, kuwa na ukabila dhidi yao, au kuwafanyia kwa misingi ya hadhi zao za kijamii, na mahali kote ambako kuna uonevu wa aina yoyote ile. Roho wa kuwakubali watu na kuwahurumia inahitaji kuonekana kati ya Wakristo wa kila kabila, rangi, na hata hadhi tofauti za kijamii. Kamwe wakristo hawastahili kuwapendelea watu au kuwabagua, bali wanahitaji kuwapenda na kuwaheshimu watu wote.

## Ukuta wa Kugawanya Watu

Kupitia kwa damu yake Kristo ukuta wa kugawanya watu kati ya Wayahudi na Mataifa ulivunjwa. Kristo

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

"Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba . . . basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu" (Waefeso 2:11-19). Basi sisi hatustahili kuwa na migawanyiko au uonevu katika familia yake Mungu, bali kwamba kila mshirika wa Kanisa anastahili kumjali mwenzake (1 Wakorintho 12:25). Kuna watu ambao wana mielekeo ya kuwabagua wale wengine kwa vigezo vya ukabila au rangi za nyuso zao, na kuwaona kwamba wao ni watu wa hali ya chini. Wayahudi waliwaona watu wa Mataifa kuwa wa cheo cha chini, lakini mtume Petro akashuhudia katika Matendo 10:28, "Mungu amenionya, nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi."



Ni makosa kuwaona watu wa tabaka tofauti kuwa hawana thamani au kwamba hawana umuhimu, kwa sababu sisi sote tuko sawa.

"Kwa kweli kubebeshwa msalaba wa maonevu ni jambo linalozua machungu, lakini Wakristo hawajapewa mweke wa kubeba kinyongo au kutosameheana."

## Tu Wamoja Katika Kristo

Hata ingawa ulimwengu unawaweka watu wengine kando na kuwagawanya, Maandiko yanatufundisha kwamba umoja ndio unastahili kutawala kati ya watu wa Mungu. "Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake" (Warumi 12:5). "Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja" (1 Wakorintho 12:13). Ili kuwe na umoja mahali ambako kuna tofauti za kimaumbile, tunahitaji kuwa na mawazo kama ya Kristo na kufuata himizo ambalo linapatikana katika Wafilipi 2:3, "Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake."

## Upendo Kati ya Ndugu

Haijalishi tofauti iliyoko kati yetu sisi Wakristo, Kristo ameamuru kwamba, "Tupendane" (Yohana 13:34). Chochote ambacho hakitokani na upendo ni dhambi, "Yeye asiyependa (ndugu yake), akaa katika mauti" (1 Yohana 3:14). Mtume Petro naye akatufundisha kwamba tuwe "wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu" (1 Petro 3:8-9). Upendo huo wa kiungu unatokana na Mungu, na ndio huangamiza mapendeleo, maonevu, ubaguzi wa rangi, na tabia za kuwaweka watu kando, n.k. Upendo wa kweli hubadilisha jinsi tunavyowaona watu wale wengine, na jinsi tunavyowatendea. Mkristo mwenye upendo wa Mungu atawaheshimu na kuwastahi watu wote.

## Kuwafanyia Watu Hukumu za Haki

Hukumu lazima ziweko maishani mwetu, lakini hukumu hizo hazistahili kufanywa kwa misingi ya ukabila au kulingana na hali za kiuchumi za watu. Sheria ya Walawi iliguzia swala hili: "Msitende yasiyo haki katika hukumu, usimpendelee mtu maskini, wala kumstahi mwenye nguvu; bali utamhukumu jirani yako kwa haki" (Walawi 19:15). Naye Kristo alitufundisha kwamba, "Msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki" (Yohana 7:24). Hebu basi tufanye hukumu ambazo misingi yake ni ukweli, sio zile ambazo misingi yake inatokana na fikra ambazo hazina msingi, fikra za kuwabagua watu wale wengine.

## Msimamo wa Mtu Binafsi Dhidi ya Ubaguzi

Ni jambo la huzuni kwamba watu wengine daima hawatafanyia wenzao mambo ya haki, upendo, na heshima; mambo ambayo ndiyo yanayofundishwa katika Biblia. Lakini Wakristo wanahitaji kufuata mafundisho ya Biblia, bila kufuata yale yanayofanyika katika jamii. Neno la Mungu linatoa mwongozo ya kile Waristo wanahitaji kufanya, wakati ambapo wamefanyiwa mambo yasiyo ya haki na ya uonevu. Kwa njia iliyo wazi kabisa, Yesu alitufundisha kwamba tuwasamehe wanaotukosea. "Kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu" (Marko 11:25-26). Kwa kweli kubebeshwa msalaba wa maonevu ni jambo linalozua machungu, lakini Wakristo hawajapewa mweke wa kubeba kinyongo au kutosameheana. "Angalieni mtu awaye yote asimlipe mwenziwe mabaya kwa mabaya" (1 Wathesalonike 5:15). Badala ya kulipiza kisasi, Yesu alituamuru kwamba "Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, wabarikieni wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi" (Luke 6:27-28). Kama vile ambavyo kuna uonevu mwingi ulimwenguni, ndivyo ambavyo kuna chuki nyingi. Basi Mkristo anahitaji kuwa macho wakati anapofanyiwa mambo yasiyofaa ili kwamba, "Shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo" (Waebrania 12:14-15). Kama jinsi ambavyo tabia za kuwabagua watu wale wengine huwa zinapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ndivyo ambavyo machungu ya moyo yanavyopitishwa. Lakini hatutaweza kuingia mbinguni kama tutakuwa watu ambao wangali wamejaa maonevu na machungu moyoni.

## Sisi Sio wa Ulimwengu

Yesu alimwomba Mungu kwamba awadumishe wanafunzi wake dhidi ya ulimwengu huu mwovu (Yohana 17:15). Uovu umejaa katika jamii; na kuna migawanyiko mikubwa katika nchi tofauti kwa misingi ya kikabila, dini, rangi za nyuso za watu, hali zao za kiuchumi n.k. Lakini watoto wa Mungu wanahitaji kuishi kwa viwango ambavyo ni vya kiwango cha juu zaidi, wao hawastahili kuishi kulingana na mambo yanayotokana na umwili. Mambo ya kilimwengu hayahitaji kuigizwa kanika Kanisa lake Mungu. Wakristo hawastahili "kuifuatisha namna ya dunia hii" (Warumi 12:2), na pia hawastahili kufuata taratibu za dunia hii na maovu yake. Badala yake wao wanastahili kuwa mfano bora wa upendo kwa watu wale wengine, kuwaheshimu, kuwapa stahili zao, msamaha, na hata kuwakubali. Hakuna nafasi ya kuwa na uonevu na kinyongo Kanisani. Hebu basi Mungu amsaidie kila Mkristo ili aepuke mielekeo hiyo ya kilimwengu ambayo ina umwili mwingi, na badala yake tuenende kwa njia za utakatifu. Njia ya usawa na kuwakubali watu wale wengine ndio njia ya kweli, haki, na ambayo inawavutia watu wale wengine. ■

# Maswali na Majibu



## Je, Biblia Inafundisha Nini Kuhusu Mtu Kumwoa Mtu Asiye wa Rangi au Taifa Lake?

Sheria ya Agano la Kale iliwakataza wana wa Israeli kuoa watu walioishi katika nchi ya Kanaani (Kutoka 34:14-16). Mungu aliwambia Waisraeli kuwaangamiza watu waliodumu humo, na pia wasioane nao. Lakini Mungu alitoa sababu ya amri hiyo yake, na sababu hiyo haikutokana na maswala ya ukabila au rangi ya nyuso zao. "Binti yako usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake. Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya BWANA juu yenu, naye atakuangamiza upesi" (Kumbukumbu 7:1-4). Mungu alitaka watu wake wawe watakatifu na waliotengwa kwa ajili yake, ili wapate wamwabudu Yeye peke yake.

Wana wa Israeli walipoanza kuoana na watu wa mataifa na makabila yale mengine, na hivyo kukosa kumtii Mungu, ndipo walianza kupata athari za ibada za sanamu na za kipagani. Nao manabii wakahubiri dhidi ya jambo hili (Malaki 2:11; Ezra 9:1-2). Kwa sababu ya kuchanganyika na watu wa nchi hizo, mioyo yao ilivutwa mbali na Mungu. Mfalme Solomoni ndio mfano wa kuhuzunisha sana wa jambo hili. "Mfalme Sulemani akawapenda wanawake wengi wageni, pamoja na binti yake Farao, wanawake wa Wamoabi, na wa Waamoni, na wa Waedomi, na wa Wasidoni, na wa Wahiti, na wa mataifa BWANA aliyowaambia wana wa Israeli, Msiingie kwao, wala wasiingie kwenu; kwa kuwa hakika wataigeuza mioyo yenu kuifuata miungu yao . . . kwa kuwa Sulemani akamfuata Ashtorethi, mungu mke wa Wasidoni na Milkomu, chukizo la Waamoni" (1 Wafalme 11:1-5).

Basi amri hiyo ya kuwakataza wana wa Israeli kuoa watu hao wa kigeni kamwe haikuhusiana na tabaka zao, bali ilihusika na athari ambazo wao wangewaletea Wayahudi, athari za ibada za sanamu. Agano Jipya nalo linatufundisha mwongozo ambao unafanana na huo, "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini?" (2 Wakorintho 6:14-15). Kwa kweli ndoa ni uhusiano wa karibu sana wa kibinadamu, na Agano Jipya linatufundisha kwamba muumini hastali kumwoa mtu ambaye si muumini; lakini msingi wa amri hii sio swala la ukabila au rangi ya nyuso za watu.

Musa naye alimwoa mwanamke Mumidiani, na baadaye akamwoa mwanamke kutoka Ethiopia. Nao Miriamu na Aaroni wakaongea dhidi ya Musa na ndoa hizo zake. Naye Mungu akawakasirikia sana, lakini Yeye hakumkasirikia Musa kwa kuoa wanawake hao, hata ikafikia kwamba Miriamu akapata ukoma kwa sababu ya hayo makosa yake (Hesabu 12:1, 9-10). Lakini upinzani huo wa Aaroni na Miriamu ulitokana na na mashindano ya mamlaka na uongozi wa wana wa Israeli dhidi yake Mungu, chanzo chake cha halisi hakikuwa ndoa hizo za Musa. Naye Albert Barnes, ambaye alikuwa mnenaji wa maoni kuhusu Biblia aliandika na kusema:

> Ndoa ambayo Musa alifanya na mwanamke wa uzao wa Hamu haikuwa imekatazwa, mradi mwanamke huyo hakuwa wa uzao wa Kanaani; lakini kwa kweli ndoa hiyo haikuwa budi kuwakasirikisha Wayahudi, kwa maana wao walikuwa na hisia kali za utaifa. Mababu wa dini ya Ukristo nao wameonelea kwamba ndoa ambazo Musa alifanya (baadaye) na yule Mumidiani, pamoja na mwanamke wa Ki-ethiopia, ilikuwa ni ishara kwamba watu wa Matafaifa mwishowe watapelekewa agano na ahadi zake Mungu.

Na katika Agano Jipya tunapatana na watu wa mataifa wa aina tofauti tofauti, "Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye yule ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao" (Warumi 10:12). Yule mwanamke Ruthu, na pia kahaba Rahabu, waliunganishwa na kizazi chake Kristo. Basi ni kweli kwamba "Alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja" (Matendo 17:26). Agano Jipya kamwe haiwakatazi watu wa utaifa tofauti kuoana.

Ndoa ni jambo muhimu sana, na kuna mengi ya kuwaza kabla ya mtu kufanya uamuzi wa ataoa nani. Kuoa ni jambo linahitaji kufanywa baada ya mtu kuomba sana na kupata mawaidha mazuri. Imani katika Kristo ndilo jambo muhimu kabisa, na sio maswala ya ukabila au rangi ya uso ya yule anayeolewa. Hivyo ndivyo ambavyo Biblia inafundisha kuhusu vile mtu anahitaji kuchagua atakayeoa. Lakini maswala ya utaifa, utamaduni, mitindo, hadhi ya kijamii ya yule anayeolewa, kabila, na hali yake ya kiuchumi n.k. ni mambo ambayo mtu anahitaji kuwaza kwa maombi kwa kulingana na hali ya utamaduni ambao anayeoa ametoka. Uhusiano wa kifamilia, misukumo ya kijamii, na vile watoto watakaozaliwa watakavyopokelewa ni mambo ambayo mtu anahitaji kuwaza kuhusu. Katika tamaduni zingine, kuna shida kubwa ambazo zinaweza tokana na mtu kufanya ndoa na mwenzake wa utaifa tofauti, jambo ambalo linaweza kufanya ndoa kama hiyo kupata magumu. Lakini hii si kusema kwamba ukimwoa mtu wa taifa lingine hiyo ni dhambi, bali ni swala la mtu kuwa na hekima na kuhakikisha kwamba anayeoa ni mtu ambaye mtasikizana; na hili ni jambo ambalo linajidhihirisha kwa njia tofauti kwenye mahali tofauti tofauti na katika hali tofauti tofauti.

KODI MUKUDZIWA?

Uonevu ni jambo ambalo limesambaa kote ulimwenguni, na ni shida ambayo inaendelea kukita mizizi ulimwenguni kote. Hii ni kulingana na takwimu kutoka World Justice Project data (Mradi wa Kitaifa wa takwimu kuhusu maswala ya haki) . . . na imepatikana kwamba katika asimilia 70% ya nchi za dunia uonevu umeongezeka katika miaka ya 2021 na 2022. Na kutoka hapo 2015, uonevu umeongezeka kwa kila thuluthi tatu ya nchi kati ya nne ambazo kikundi cha WJP kilifanya utafiti wake.

(2023, Machi 21). Discrimination is Getting Worse Globally (uonevu unaendelea kuzidi ulimwenguni kote). www.worldjusticeproject.org

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# KITAMBULISHO CHETU NDANI YAKE KRISTO

*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu.* —1 Petro 2:9

Wana wa Israeli walikuwa watu waliochaguliwa na Mungu, na wao walikuwa watu spesheli kwa Mungu, watu wenye hadhi iliyokuwa ya kiwango cha juu zaidi ya watu wale wengine. Wao walitengwa na mataifa mengine ili kwamba wamwabudu Mungu peke yake. Mapenzi ya Mungu ilikuwa kwamba wao wadumishe kitambulisho chao ili wasitiwe dosari na ibada ya sanamu za mataifa yale mengine. Mungu aliwataka walinde na kuutetea urithi huo wao kwa vyovyote vile. Wayahudi walikuwa na kitambulisho maalum kama watu wa thamani kwake Mungu.



Lakini Yesu Kristo alikuja na kuwapatanisha watu wote na Mungu kupitia kwa damu yake. Sisi hupokea msamaha wake Mungu na kuokolewa kutokana na nguvu za dhambi, na tunafanyika viumbe vipya. Tunapata kitambulisho kipya cha ajabu katika Yesu Kristo, kama raia wa ufalme wa Mungu. Basi sisi tumechaguliwa, na sisi tu makuhani wa kifalme.

Kwa kweli watu wa ulimwengu wanatafuta "kitambulisho." Kuna watu walio na kiburi na ubaguzi dhidi ya wale wengine. Watu wanapokuwa na mielekeo kama hiyo, sababu yake mara nyingi huwa kwamba wao hawana amani ndani ya mioyo yao. Wakati mtu amemkosea heshima mwenzake kutokana na chuki, kutojihisi salama, ubinafsi, kiburi, tamaa, kuamini habari isiyo sahihi, na kutokujua, hii ni kuonyesha kwamba aliye na mwelekeo kama huo kitambulisho chake huwa kimejengwa juu ya msingi ambao haufai.

Hata ingawa sote tuna urithi wetu wa kabila zetu na mataifa yetu, kitambulisho chetu halisi kinapatikana ndani yake Mungu, na sisi tu wana wa Mungu, kwa maana hapo ndipo tunapopata pumziko la kweli. Watu wengi hupata ugumu kujikubali, na hata kuona vigumu kuikubali hata rangi za nyuso zao. Lakini Mungu anataka tukubali vile ambavyo alituumba, na tuwe na amani kwa jambo hilo. Sisi tumechaguliwa na Mungu, na hatuna haja ya kukazana kupata kitambulisho kingine ambacho si cha kweli, jambo ambalo ni shida kubwa katika ulimwengu wa sasa. Kitambulisho chetu ndani yake Kristo ndicho ambacho kitakachotuongoza hadi tufike huko makao yetu ya milele! ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA